Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Wilayah Sudan

Jumanne, 17 Rabi' I 1447 H | 09/09/2025 M | Na: HTS 1447 / 29

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

**Ujumbe kutoka Hizb ut Tahrir / Wilayah Sudan**
**Wakutana na Mkurugenzi wa Khalawi na Idara za Misikiti katika Mji wa Port Sudan**
**(Imetafsiriwa)**

Ujumbe kutoka Hizb ut Tahrir/Wilayah Sudan ukiongozwa na Ustadh Nasser Ridha Mkuu wa Kamati Kuu ya Mawasiliano ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah ya Sudan akifuatana na Ustadh Abdullah Ismail Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano, ulimtembelea Sheikh Onour Muhammad Ahmed, Mkurugenzi wa Khalawi na Idara za Misikiti katika Mji wa Port Sudan, afisini kwake, kama sehemu ya kampeni iliyoandaliwa na Hizb kutibua njama ya kuichana Sudan kwa kuitenganisha Darfur.

Ustadh Nasser alizungumzia yanayojiri hivi sasa nchini Sudan mikononi mwa makafiri wa Magharibi hasa Amerika iliyotenganisha Sudan Kusini, na sasa inataka kuitenga Darfur, kisha hatua inayofuata ni Sudan Mashariki. Jambo hili ni miongoni mwa masuala muhimu, na miongoni mwa masuala nyeti, ambayo ndani yake hakuna upole, na ambayo yanahitaji kutoka kwa maimamu wa misikiti, na kutoka kwa wanasiasa, wanafikra, viongozi wa jeshi, na watu kwa jumla, kufanya kazi kwa umakini ili kukwamisha mpango huu. Ustadh Nasser alitoa ushahidi kadhaa kuthibitisha kile alichokitaja.

Sheikh Onour alithibitisha maneno ya Nasser na kusema: "Je, dori yetu ni ipi?" Ustadh Nasser akamueleza kile kinachotakiwa kutoka kwa maimamu na wahubiri, na Sheikh akaomba kwamba mpango wa Hizb wa kutibua njama nzima upelekwe kwake.

Mkutano huo pia ulihudhuriwa na Naibu Mkurugenzi wa Afisi hiyo, Sheikh Lubab, Mjumbe wa Mamlaka ya Wanazuoni wa Wilayah na Sheikh Al-Tayeb Al-Shambali, Mkurugenzi wa Masuala ya Wenye Kuhifadhi Quran katika Jimbo la Bahari Nyekundu.

**Ibrahim Othman (Abu Khalil)**
**Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir**
**Wilayah Sudan**

**Simu:** 0912240143- 0912377707

**Pepe:** Spokman_sd@dbzmail.com

**Tovuti:** www.hizb-sudan.org

**Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:** www.hizb-ut-tahrir.org

**Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:** www.hizb-ut-tahrir.info